



# **Fasihi-Simulizi – Methali 8**

*Luhala lwa Wavidunda*

**Hekima ya Kividunda**

*N'heko dza Chividunda  
Methali za Kividunda*

**Kividunda kwa Kiswahili na  
Kiswahili kwa Kividunda**

Karsten Legère na Peter S. Mkwan’hembo  
(wahariri)  
Dibaji: Shani Omari Mchepange

Michoro: Juma Mgenda

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili  
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili  
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam  
S.L.P. 35110  
DAR ES SALAAM

Vidunda Proverbs plus Swahili equivalents

Editors. Prof. Dr. habil. Karsten Legère and Peter S.  
Mkwan'hembo

Contributed by:

- (1) †Mzee Simon Maganga
- (2) Mzee Martin Protas
- (3) Adrian M. Kaugala
- (4) Pius Kaugala Chihuku
- (5) †Mama Edmunda Matajiri
- (6) Dafrosa Mkwan'hembo
- (7) Paskal Msomoze

Foreword: Shani Omari Mchepange, Ph. D.

Illustrations: Juma Mgenda

© Karsten Legère and Peter S. Mkwan'hembo 2019

ISBN: 978-9976-5316-5-7

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki au sehemu ya kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya wahariri na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

## Dibaji

Semi kama kipengele kimojawapo cha fasihi simulizi, zimefumbata ukwasi usiomithilika. Kupitia vitendawili, nahau, misemo, na methali kwa namna ya pekee, jamii imekuwa ikipata mwongozo wa namna ya kuenenda katika maisha. Kwa muda mrefu methali zimekuwa zikiitwa ‘semi zenye hekima na busara.’ Hii ni kutohana na ukweli kwamba wazazi, walezi na watu wengine katika jamii wamekuwa wakizitumia katika kuwafunda watoto na vijana na hata watu wa marika mengine katika mambo kadha ya maisha.

Kila mara katika muktadha wa mazungumzo yenye mwelekeo wa kufunda, neno ‘wahenga’ linapotamkwa limekuwa likifuatiwa na methali fulani yenye dhima maalumu ya kuonya, kuadibu, kuelimisha na kadhalika. Mathalani, mtoto au kijana anapoonekana kwenda kinyume na maadili ya jamii huweza kuambiwa, “Wahenga walisema, ‘Asiyesikia la mkuu huvunjika guu’.” Wahenga katika muktadha huu huchukuliwa kama watu wa kale wenye hekima, busara na maarifa wanaotegemewa katika mashauri. Ni kwa namna hiyo methali (tungo zenye hekima na busara) hunasibishwa na wahenga.

Kitabu hiki cha Methali za Kividunda ni matokeo ya utafiti uliofanyika katika jamii ya Wavidunda inayopatikana mkoani Morogoro, nchini Tanzania. Hii inadhihirisha kuwa kuna utajiri mwingi wa semi katika fasihi za makabila mbalimbali. Licha ya methali zilizozoleka katika Kiswahili, kuna methali nyingine nyingi za jamii mbalimbali ambazo zikitafsiriwa kwa kuzingatia kanuni za kimethali na ujumi wake, zitasaidia kutunisha kapu la

methali za Kiswahili tulizo nazo hivyo kuzidi kujiongezea utajiri.

Kwa sababu ya utajiri huo na dhima ya methali katika jamii, kitabu hiki kina manufaa makubwa kwa jamii. Methali hizi zitasaidia kutunisha kanzidata ya methali za Kiswahili zilizopo na kupenyeza hekima na busara zilizochotwa kutoka katika jamii ya Wavidunda katika fasihi pana ya Kiswahili. Fauka ya hayo, kitabu hiki kitawasaidia watafiti wa aina mbalimbali wanaoshughulika na fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo, kukamilika kwa chapisho hili ni chachu kwa watafiti wengine kufanya tafiti za methali katika jamii nyingine na kutoa machapisho yatakayosaidia kupanua wigo wa semi hususan methali za Kiswahili.

Kwa namna ya pekee, nawapongeza wahariri wa kitabu hiki, Karsten Legère na Peter S. Mkwan'hembo waliojijusurisha kufanya utafiti na kuandaa mswada wa kitabu hiki. Aidha, pongezi kwa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) kwa kuchapisha kitabu hiki katika jitihada zake za kuendeleza lugha ya Kiswahili na fasihi yake. Shime!

Dkt. Shani Omari Mchepange

Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji Taasisi ya Taaluma za Kiswahili

Tarehe: 27/08/2019

## **Utangulizi**

Kitabu hiki ni mchango mwagine ambao unatokana na utafiti wa uwandani uliofanyika mionganoni mwa Wavidunda waliopo katika Kata ya Vidunda, Wilaya ya Kilosa (Mkoa wa Morogoro). Huko ndiko kitovu cha matumizi na uendelezaji wa lugha yao ya Chividunda (lugha ya milima) ambayo huzungumzwa katika vijiji vya Vidunda, Udung'hu na Chonwe. Idadi ya wazungumzaji wake inakadiriwa kuwa ni watu 12,000. Wavidunda wengine wanaoishi bondeni na mahali pengine wilayani humo hawazungumzi sana lugha hiyo. Hii ni kutokana na uwepo wa mwilingiliano wa lugha mbalimbali ambao umewafanya wananchi hao watumie lugha ya Kiswahili kwa mawasiliano nje ya jamii husika.

Mwelekeo wa kusanyiko hili la fasihi-simulizi ya Kividunda ni kuwaletenee wasomaji mifano ya methali ambazo Wavidunda huwa wanazitumia hadi sasa. Kwa upande mmoja, asili ya methali hizo nyingi bado haijulikani, ila tunajua kuwa zilizuka zamani. Kwa upande wa pili, hadhi na umuhimu wa lugha ya Taifa ziliwafanya Wavidunda wafasiri hekima na busara ya methali za Kiswahili kwa kuunda visawe katika Kividunda. Kwa namna yake methali zinazotumiwa na Wavidunda na kutolewa katika kitabu hiki zinaonyesha urithi mkubwa wa kijadi uliopo katika jamii. Isitoshe, jamii hiyo huwa tayari kupokea urithi wa kitaifa unaoenezwa kwa lugha ya Taifa. Kwa kufanya hivyo, kusanyiko hili ni mfano wa kuigwa wa kukaribisha wananchi wengine kwenda na wakati kwa

kutajirisha lugha yao na methali za mkopo zenyе asili ya Kiswahili.

Kitabu chetu hiki kina sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni lugha asilia ya methali za Kividunda zinazofuatiwa na ufanuzi mfupi wa Kiswahili au, ikiwezekana, kisawe chake katika lugha hiyo. Sehemu ya pili ni ile ya Kiswahili kwa Kividunda. Inafaa kudokeza hapa kuwa ujumbe wa methali fulani katika lugha nyingine si rahisi. Inavyoonekana ni kuwa methali nyingi kiasi za Kividunda pamoja na hekima na busara zilizojumuishwa humo ndani hutafsiriwa kwa kifupi, kwa vile hata bingwa wa lugha ya Kiswahili kama M. Mwinyi (msanifu lugha mstaafu wa Baraza la Kiswahili la Taifa) alipendelea kufanya hivyo. Hii inamaanisha kuwa juhudzi za kuchambua methali asilia na kuziwakilisha barabara kwa methali za Kiswahili yapaswa zichukuliwe ili hatimaye urithi wa vizazi vilivyotangulia vya Kividunda upatikane kitaifa. Kwa kweli kitabu hiki ni moja kati ya hatua nyingine muhimu sana ya kuhifadhi kwa maandishi urithi huo.

Historia ya kukusanya, kunukuu, kuhariri na kuchapisha fasihi-simulizi za Wavidunda si ndefu. Hata shughuli za kukusanya na kuweka kumbukumbu za methali ni za hivi karibuni tu kwa sababu mbalimbali ambazo haziorodheshwi hapa. Kilichokuwa muhimu ni ile ari ya Wavidunda kadhaa ambaao walikutana na kuanza kurikodi methali kama ilivyokuwa awali wakati pale wazee wao walipokuwa wakisimulia hadithi hizo kwa wingi. Ushirikiano mwema na wahariri ulisaidia pande zote mbili kufanikisha mradi huu. Shukrani za pekee ziwaendee wazee akina hayati Simon Maganga, Martini Perotasi,

hayati Bi Edimunda H. Matajiri na aila yake, Bi Katalina Visenti, hayati Yusti Mayuga na wengine pamoja na watoto ambaao baadaye walijitolea kukusanya, kukariri na kuzifafanua methali hizo. Isitoshe, hao wote walirahisisha sana kazi za wahariri ambaao kwa pamoja walihakikisha kuwa muswada uliorekebishwa na kupanuliwa hatua kwa hatua unatungwa. Kwa upande wa Kiswahili, Bi Rahma Muhdhar (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) na Bw. Mohamed Mwinyi walisoma na kupiga msasa muswada na utangulizi wake. Bila ya kumsahau mwenzetu mwaminifu Bw. Juma Mgenda ambaye kama kawaida yake alichora michoro ya kupendeza inayodhihirisha vizuri maana ya methali. Wahariri wanawashukuru wote waliotajwa hapo juu pamoja na wengine waliotusaidia ambaao majina yao hayakuweza kutajwa hapa.

Wanataaluma wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili nao pia walichangia sana kufanikisha muswada huu na kuutayarisha kwa uchapishaji. Shukrani za pekee ziwaendee Prof. Mstaafu Mulokozi na Dkt. Shani Omari ambaao waliandika uhakiki uliosaidia sana maendeleo ya shughuli za kupokea muswada TATAKI. Isitoshe, Dkt. Musa Hans alifuatilia kwa makini kazi za ndani ya TATAKI zilizohusika na maandalizi ya uchapaji wa siku zijazo. Ahsante sana, Dkt. Hans, Dkt. Shani Omari Mchepange (mtunga dibaji) pamoja na wenzenu wote wa TATAKI mliokuwa nasi katika kupiga hatua za mwisho za matayarisho ya upigaji chapa wa muswada mzima.

Mwisho kabisa, tunapenda kuwataarifu kwamba utafiti uwandani pamoja na ushirikiano na Wavidunda (hasa wa kijiji cha Vidunda) wakati wa shughuli za mradi wa Luga

za Tanzania uligharimiwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Kiswidi (SIDA). Katika mradi huo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Idara ya Lugha za Kigeni na Isimu pamoja na Chuo Kikuu cha Gothenburg, Idara ya Lugha na Fasihi zililifuatilia kwa makini uwezeshwaji wa lugha nyingi mbali na lugha ya Taifa ya Kiswahili. Mmojawapo wa wahariri ambaye kwa miaka kumi alikuwa Profesa (sasa mstaafu) wa Chuo Kikuu cha Gothenburg anathamini sana msaada huu.

Sisi wahariri tunawatakieni wasomaji wa kitabu hiki cha methali za Kividunda mapokezi mazuri, usomaji wa furaha na mafunzo mema kwa amali bora zinazojitokeza katika kitabu hiki.

Karsten Legère Peter  
Dar es Salaam, Vienna, Agosti 2019

## **Yaliyomo**

Dibaji..... i

Utangulizi..... iii

N'helο dza Chividunda kwa Chiswahili

*Methali za Kividunda kwa Kiswahili .....* 3


*Methali za Kiswahili kwa Kividunda*

N'helο dza Chiswahili kwa Chividunda..... 39




**N’helο dza Chividunda kwa Chiswahili**  
*Methali za Kividunda kwa Kiswahili*





1. Bendela yangufata balidi.  
*Bendera hufuata upepo.*
2. Cha hasi chiting'anaga na cha mchany'ha.  
*Cha chini hukutana na cha juu.*
3. Cha miyago chikangafu, umele mate, ukawase.  
*Cha mwenzio kitaalamu, umeze mate, ukalale.*
4. Cha mun'hu chinung'ha mvili.  
*Cha mtu kinanuka nywele.*



5. Chaluko cha n'honya ng'hungugu.  
*Dalili ya mvua ni mawingu.*



6. Chideje chigwaga migodi ho chiganile.  
*Ndege hutua kwenye miti aupendao.*
7. Chideje chisugu chogwilila mchitubuli chihalibiche.  
*Ndege mjanja hunaswa kwenye tundu bovu.*

8.




Chidole chimwe  
hachitulaga mp'hani.  
*Kidole kimoja  
hakivunji chawa.*

9.



Chidole chinojile  
chovalidzwa pete.  
*Chanda chema  
huvikwa pete.*

10. Chidzanga cho hudile chokwawa choni?  
*Pilipili usiyoila yakuwashiani?*
11. Chigana n'humbulu mkwandi.  
*Kipendacho roho ni dawa.*
12. Chigune cha mayowe, mp'helasi dzahela chigune.  
*Kigune ni cha karanga, njugu mawe hazina kigune.*
13. Chikunde mbala mwamidzi Mulungu.  
*Mtu mwenye shida mlinzi wake Mola.*
14. Chila chideje changuguluka kwa ibawa lyache.  
*Kila ndege huruka kwa bawa lake.*
15. Chila lwidzi na funguwo yache.  
*Kila mlango kwa ufunguo wake.*
16. Chila mwana na likoja lyache.  
*Kila mtoto na koja lake.*
17. Chilawile kwa mutwa, ubochele.  
*Kilichotoka kwa mkarimu, upokee.*
18. Chililo chalukaga yafililwe, leka wanji wa kutali wenjile.  
*Kilio huanza mfiwa ndipo wa mbali waingie.*



19. Chin'handa cho huwasile, hujidzelele mikugun'hi jake.  
*Kitanda usicholala hujui kunguni wake.*


20. Chin'hu chinojile chonekaga, idzuwa lilawila.  
*Kitu kizuri kinaonekana, juu linapochomoza.*
21. Chin'hu chiteleche somba, hachileka kunung'ha udzidziwa.  
*Chombo kilichopikiwa samaki hakiachi kunuka vumba.*
22. Chinojile changigudza, chichile changijendedza.  
*Kizuri chajuza, kibaya chajitembeza.*
23. Chitumagwa hakopolagwa.  
*Mjumbe hauawi.*
24. Chivuli cha ng'hweku hachimvisa mun'hu idzuwa.  
*Kivuli cha fimbo hakimfichi mtu juu.*
25. Dzuko, dzuko vyotulutaga.  
*Twende, twende tunavyoenda.*
26. Ga katali, ga kuduhi.  
*Ya kale hayapo.*
27. Hakucha, hakucha kucha.  
*Hauchi, hauchi unakucha.*
28. Hali usungu hamwaka hana chilyo.  
*Penye machungu baadaye pana chakula.*
29. Halina luhuwi, hana ndzila  
Haweles na niya, ndzila yowa baho.  
*Penye nia, pana njia.*
30. Hasala yomfika yula yawele nambedza.  
*Hasara humfika yule mwenye mabezo.*
31. Hasila dza mkidzi, ny'hendze ya mlowaji.  
*Hasira za mkizi, furaha ya mvuvi.*

32. Hasila hasala.  
*Hasira hasara.*
33. Hawele na wadahile hawakosaga wakifundza.  
*Penye mafundi hapakosi wanafunzi.*




34. Hawele na wadzehe haiharibikaga mbuli.  
*Penye wazee haliharibiki neno.*
35. Hehile hako siyo hanojile ha miyago.  
*Pabaya pako si pema pa mwenzako.*

36. Heli ufe meho kuliko kufa n'humbulu.  
*Heri kufa macho kuliko kufa moyo.*
37. Heli wikkale chidole kuliko kikwala lulimi.  
*Heri kujikwaa kidole kuliko kujikwaa ulimi.*
38. Hima, hima yahela mboto.  
*Haraka, haraka haina baraka.*
39. Hiiali yangusinda utumwa.  
*Hiari yashinda utumwa.*
40. Ibugulu siyo chin'hu.  
*Wingi siyo kitu.*
41. Iduwa lihile hatambichidzagwa mwana.  
*Dua mbaya haombolezewi mtoto.*



42. Idzogolo lya kumugunda halikwika kump'hwani.  
*Jogoo wa shamba hawiki mjini.*
43. Idzogolo lyadzimwa lilumaga dzing'hulu na dzinyana.  
*Jogoo wa kuazima anauma wakubwa na wadogo.*


44. Ifigwa limwe halijeleka chiya.  
*Jifya moja halinjiki chungu.*
45. Ifulusi lya miyago ni chikanda cha sufi.  
*Mzigo wa mwenzio ni kanda la sufi.*
46. Ifumbo mfumbile mpoka, yawele na luhala ama kalitanga.  
*Fumbo mfumbie mjinga, mwerevu huling'amuia.*
- 47.




Ihuka halimtagaga  
mun'hu.  
*Jembe halimtupi mtu*  
(mkulima).

48. Ikanga halilela kuujendzi.  
*Kanga hazai ugenini.*
49. Ikune ibende, ujende nimwanimwa, wan'hu wakutogole.  
*Pania nguo, uende huku na kule, watu watakusifu.*

50. Imaka uhome kwa mun'hu lya usungu.  
*Mnyama mchome kwa mtu mwenye uchungu.*




51. Ing'oko linyamalile lo lipataga ndiya.  
*Mnyama mkimya ndiye anayepata chakula.*  
*Mvumilivu hula mbivu.*



52. Inyau woné lyuche, igule lyohalila.  
*Paka akiondoka, panya hutawala.*
53. Isi ibende, mwenye ngoma dzake uleche yadule.  
*Dunia tambara mbovu, mwenye ngoma zake asicheze.*
54. Isi igodi ikavu.  
*Dunia mti mkavu.*

55. Isi ilihela wakulu, haiwaga.  
*Nchi iliyokosa wakubwa inakosa ustawi.*
56. Isichiyo haliwasaga na ndzala mwemvu.  
*Sikio halilali na njaa.*
57. Itagwa linojile lyangung'ala kutitu.  
*Jina jema hung'aa gizani.*
58. Ituli hawatwangaga bila chin'hu.  
*Kinu hakitwangwi bila kitu.*
59. Iwago lilihela chaka haitema ngodi.  
*Shoka lisilo na mpini halichanji kuni.*
60. Iyungu likulaga hima hima na idenje hihyo.  
*Boga linakua haraka haraka, mwanzo hivyo hivyo.*



61. Kadzanda kado kamema mimamba.  
*Mto mdogo umejaa mamba.*
62. Kagunda kado kalimwa na wan'hu wenji.  
*Shamba dogo limelimwa na watu wengi.*

63. Kanguseka ng'hou yang'alifichikwa na chilonda.  
*Hucheka kovu asiyefikwa na jeraha.*




64. Kapene kachiwa kedimaga kali yeng'ha.  
*Mbuzi mkiwa anajichunga peke yake.*
65. Kibiha kwinji, kokuka na mamvi.  
*Kuchamba kwingi, kuondoka na mavi.*
66. Kikala kwinji, kolola menji.  
*Kuishi kwingi ni kuona mengi.*
67. Kikwala siyo kugwa, kuluta kumwando.  
*Kujikwaa si kuanguka, bali ni kwenda mbele.*



68. Kisubula kwa mipandzi ny'hendze dla mibondwa.  
*Vita vya panzi furaha ya kunguru.*

69. Ko uswese, ko ulya.  
*Ulikoshinda ndiko utapata chakula.*
70. Ko yawasila kota idimu, ko undza mane.  
*Alipolala kama zimwi, unakoenda, hujui.*
71. Kochidzada ha hadzadagwa.  
*Utajikuna pasipokunwa.*
72. Kohanga na wegute (wokukombela), wokusindila mboga.  
*Ukishirikiana na walioshiba (watakomba), wanakumalizia mboga.*
73. Kokula kovyona, ukulu hauvinaga.  
*Utakuwa utaviona, ukubwa hauchezi.*
74. Kokwima n'honje, hokwima ineno.  
*Hukunyima tongue, hakunyimi neno.*
75. Kosoka lili mp'halika, lyolawa, lyokulumा.  
*Utakachokonoa lililoko kwenye pango, litatoka, litakuma.*



76. Kotaga ng'hwabi na ipela lyake.  
*Usitupe jongoo na mti (mpera) wake.*
77. Kotowa, halinalawa.  
*Utapiga, bado halijatoka.*
78. Kubetedzabetedza kwangulumidza munda.  
*Ngojangoja yaumiza matumbo.*

79. Kuduhu hajali ikosile miyage.  
*Hakuna msiba usio na mwenzake.*



80. Kuduhu sili ya wan'hu weli.  
*Hakuna siri ya watu wawili.*
81. Kufa kwa mun'hu nyemi.  
*Kufa kwa mtu sherehe.*
82. Kuhomba igwingwi na igodi lyake.  
*Usitupe jongoo na mti wake.*
83. Kuhulula kwa idebe mp'humu ya mpikaji.  
*Kuvuja kwa pakacha nafuu ya mchukuzi.*
84. Kulavya chin'hu n'humbula, siyo utajili.  
*Kutoa ni moyo, si utajiri.*
85. Kuli migodi minji wan'hu wa kudzenga kuduhu.  
*Penye miti mingi hakuna wajenzi.*

86. Kuluta hima hima siyo kufika.  
*Kwenda mbio siyo kufika.*



87. Kumeho kuwumbigwa na soni.  
*Uso umeumbwa na haya.*


88.



Kutundza himila  
siyo m jit o, mijito  
kutundza mwana.  
*Kulea mimba siyo  
kazi, kazi kulea  
mtoto.*

89. Kuwudza siyo upoka.  
*Kuuliza si ujinga.*
90. Kwajilila ndzila ndo kuidzela ndzila.  
*Kupotea njia ndiyo kujua njia.*

91. Lehano yo lehano, yolenga cheso mdesi.  
*Leo ni leo, asemaye kesho ni mwongo.*
92. Lidimu likudzelele halikulya, lisinde.  
*Zimwi likujualo halikuli, likakwisha.*



93. Lidzeleche mmadzi menji li papa, kumbe jiyage jilikuko  
*Avumaye baharini ni papa, kumbe wengine wapo.*
94. Likosa limwe halilekaga mdala.  
*Kosa moja haliachi mke.*
95. Likwete, kamwe halitegagwa.  
*Lililopita mara moja, halitegwi.*
96. Lilonjigwa lya kuko, wone likuduhu, lya kumbele,  
lyanguya.  
*Lisemwalo lipo, ikiwa halipo, lipo nyuma, linakuja.*
97. Luhala kwa nalo kojenda, koleka, luluta.  
*Akili unayo utatembea, utaacha, inakwenda.*
98. Luhala lwa miyago ulonje.  
*Akili ya mwenzio useme.*
99. Luhala lwinji lwangusa maahalifa.  
*Akili nydingi huondoa maarifa.*

100. Luhala mbundamile.  
*Akili imejificha.*
101. Lukupe lukulu halukosaga ukwangulo.  
*Jungu kubwa halikosi ukoko.*
102. Lulimi lwangujejeda kuliko mibogogo.  
*Ulimi unatafuna kuliko meno.*
103. Lupogo ho lwinjilile ndiyo baho ho lulawila.  
*Mwiba ulipoingilia ndiyo hapo utakapotokea.*
104. Lya mchany'ha halitungulagwa.  
*La juu halitunguliwi.*
105. Lyo uligana hulipata, kolipata lila lyo wandichilwe.  
*Upendalo hupati hupata ujaliwalo.*
106. Madzi ga chiwambu, bahali ya misungusungu.  
*Maji ya kifuu, bahari ya chunguchungu.*



107. Malumbo ga idogowi mateche.  
*Shukrani ya punda mateke.*
108. Mamvi ga katali haganung'haga.  
*Mavi ya kale hayanuki.*

109. Mapendzi ng'hololo, hogowedza kivisa.  
*Mapenzi ni kikohozi, hayawezi kufichika.*
110. Masichini halokotaga, wone yalokote, wota kahidza.  
*Maskini haokoti, akiokota huambiwa kaiba.*
111. Mawudza halyaga cha mun'hu.  
*Kuuliza si ujinga.*
112. Mbata meli, limwe lyomulemwa.  
*Mshika mbili, moja humponyoka.*



113. Mbawa chisima kokwinjiла yuye.  
*Mchimba kisima huingia mwenyewe.*
114. Mbedzampedza jotumbuka mifila.  
*Mzaha mzaha hutumbuka usaha.*
115. Mbena isi ni mwanaisi.  
*Mvunja nchi ni mwananchi*
116. Mbeyaji hebeyaga, wone yebeye, kochitema.  
*Kinyozi hajinyoi, akijinyoa, hujikata.*
117. Mboko ya mnyonje mulundo.  
*Fimbo ya mnyonge ni umoja.*

118. Mbuhu kahela lukolo.  
*Mchoyo hana marafiki (hana ukoo).*
119. Mbuli yo huidzelele ayo kota jidza ya nechilo.  
*Jambo usilolijua ni kama usiku wa giza.*
120. Mdawalila midongo jomnyondzo chela.  
*Mcheza na tope humrukia.*
121. Mdovya hanombwa hadovyaga kamwe.  
*Mchovya asali hachovyi mara moja.*




122. Mdusu na mp'halika yake.  
*Mjusi na pango lake.*
123. Meho gahela paziya.  
*Macho hayana pazia.*
124. Mganga hedzundzuwikaga.  
*Mganga hajigangi.*
125. Mgongo ukupapaga ndiyo koulilila.  
*Mgongo unaokubeba ndiyo utakaoulilia.*




126. Mhagula ihuka hadahile kutowa ihuka.  
*Mchagua jembe hajui kupiga jembe (si mkulima).*
127. Mhagula nadzi kokwinula mbowa.  
*Mchagua nazi hupata koroma.*
128. Mhawi umupe mwanago, yahembule.  
*Mchawi mpe mwana, alee.*
129. Mhidzi kochibatika na mhidzi miyage.  
*Mwizi hushikwa na mwizi mwenzake.*
130. Mhidzi siku dzache alubayini.  
*Siku za mwizi ni arobaini.*
131. Mibadzuka jimugwaga mun'hu yalihela ndole dza kidzadila.  
*Upele hupewa, usikucha.*
132. Mibewa minji hajibawaga mwina ulute.  
*Panya wengi hawachimbi shimo.*

133. Mibogogo ja libwa halijilumaga.  
*Meno ya mbwa hayaumani.*



134. Midohe ja mp'hene jivilaga kuching'onda.  
Ndohe dza mp'hene dzivilaga kuching'onda.  
*Kinyesi cha mbuzi kinaongezeka kwenye zizi.*
135. Mijito jihile siyo mdawalo unojile.  
*Kazi mbaya si mchezo mwema.*
136. Mikale vyo midzelele.  
*Kaeni mnavyofahamiana.*
137. Mkola maya koka, kasejeda, kalya.  
*Mfanya ovyo akaondoka, anayefanya vizuri akala.*
138. Mkolela midzuwa kodila mchimbehelo.  
*Mfanyia juani atalia kivulini.*
139. Mlimaji yumwe, walyaji ibugulu.  
*Mkulima mmoja, walaji wengi.*
140. Mmela minji, lumelo lugadzi.  
*Mmeza mengi, koo pana.*
141. Mnyala vibi kolya vibi.  
*Mpanda ovyo hula ovyo.*



142. Moko uliyeka hawamyangaga.  
Moko yeng'ha haumyangagwa.  
*Mkono mtupu haulambwi.*
143. Mp'hanje wone iwe hela mavuwa, yangusinjidzia idzuwa.  
*Mbaazi ukikosa maua, husingizia jua.*
144. Mp'hene kuching'wenyo haikosaga kuluta.  
*Mbuzi sehemu ya kulamba hakosi kwenda.*



145. Mp'hole mp'hole mwandza wangutulika.  
*Polepole ndiyo mwendo.*
146. Mtamiche haudzagwa ibwembwela.  
*Mgonjwa haulizwi uji.*
147. Mteleka mikwandi hetele kaga yuye.  
*Mpishi wa dawa hajitibu mwenyewe.*

148. Muhele umwe, utelekaji winji (wahenji).  
*Mchele mmoja, mapishi mengi (mbalimbali).*
149. Muhenjela ng'howo igofu lya mugati.  
*Mfyeka migomba masilahi yake yamo ndani.*
150. Mulumbe wa mamo yo baba.  
*Mume wa mama ni baba.*
151. Mulungu kedzela yeka.  
*Mwenyezi Mungu anajua peke yake.*
152. Mulya hanombwa komalidza ibuyu.  
*Mla asali atamaliza kibuyu.*
153. Mun'hu halemaga kuchemigwa, kolema cho yochemelwa.  
*Mtu hakatai wito, hukataa neno.*



154. Mun'hu na miyage wedzela kwa miwende jawo.  
*Waarabu wa Pemba hujuana kwa vilemba.*


155. Muyago wone yobeigwa, nagwe udodze madzi.  
*Mwenzako akinyolewa, zako tia maji.*
156. Mwana hatundzilagwa mng'anda mwa miyago.  
*Mtoto hatunzwi kwenye nyumba ya mwenzako.*
157. Mwana kanya ng'hande, kadakulilwa na mayake.  
*Mtoto kunya kande, katafuniwa na mama yake.*
158. Mwana wa idzoka idzoka.  
*Mtoto wa nyoka ni nyoka.*
159. Mwana wone umudime, kokula hihyo.  
*Mtoto umleavyo, ndivyo akuavyo.*
160. Mwenyegawa hamvisaga mnafichi.  
*Mungu hamfichi mnafiki.*
161. Mwina wa ndzoka wawoga, mwina wa mbuku twa hamwe.  
*Shimo la nyoka lina woga, shimo la panya buku tuko wote.*
162. N'handze kuli idzuwa. Cheso ndokutadza kuli n'honya.  
*Nisaidie kwenye jua. Kesho nitakusaidia kwenye mvua.*



163. N'honya ng'hulu dzeng'ha dzina ndzugun'hi.  
*Mvua kubwa zote zina mbu.*

164. Nauchidzele cho ilya ndzuchi, hawalijedza hanombwa.  
*Ungalijua alacho nyuki usingalionja asali.*
165. Ndopa ndzito kuliko madzi.  
*Damu nzito kuliko maji.*
166. Ndzuchi ng'halu ina ulengu.  
*Nyuki wakali wana asali.*
167. Ng'hombeledza si sawa na chibalu.  
*Kukombeleza siyo sawa na kukosa kabisa.*
168. Ng'hondzi ifilaga mchilonda. Ng'hondzi kufila mchilonda siyo vibi.  
*Nzi hufia kwenye kidonda.*
169. Ng'howo chipakapaka dzipyga, wan'hu wangulemwela kulya.  
*Ndizi kipakapaka zimeiva, watu wanashindwa kula.*
170. Ng'huku haitulaga ifinga lyache.  
*Kuku havunji yai lake.*
180. Ng'huku iwele na wana haitodzelagwa iganga.  
*Kuku mwenye watoto halengwi jiwe.*

181.




Ng'huku njendzi  
 haikosaga ludzabi  
 muludzayo.  
*Kuku mgeni hakosi  
 kamba mguuni.*

182. Ng'huku won ibije mwanage, hafaga.  
*Teke la kuku halimuumizi mwanawe.*
183. Ng'hweso hudumuchila hagandile.  
*Kamba hukatikia pembamba.*
184. Ngubi kafa, kana mgonedzi.  
*Nguruwe kafa, kachongewa.*
185. Nyani na n'humbili na muhulo wao.  
*Nyani na tumbili na msitu wao.*
186. Seliya musumeno, wangutema kuno na kuno.  
*Sheria ni msumeno, hukata huku na huku.*
- 
187. Siku igoloche yonekaga usubuhi.  
*Siku njema huonekana asubuhi.*
188. Siku yo ujenda mwadzi, mo chiting'ana na mkweyo.  
*Siku utakayokwenda uchi, ndiyo siku utakayokutana na mkweo.*




189. Simba mbili habokwa nyama.  
*Simba wawili hawapokonywi nyama.*
190. Siyo jeng'ha jiwele na midole jiwaga misimba.  
*Siyo kila mwenye makucha huwa ni simba.*



191. Somba uibine ing'hali ndodi.  
*Samaki mkunje angali mbichi.*

192. Tudo, tudo komemedza chidoto.  
*Haba na haba hujaza kibaba.*
193. Udeche ulyagwa.  
*Ukarimu unaliwa.*
194. Ujende, ulole isi, ina kwalo.  
*Tembea, uone nchi, ina matatizo.*
195. Ujimbi ngule haumalaga.  
*Pombe ya kuuza haiishi.*
196. Ukalalile hoikwalile, siyo hougwile.  
*Ukasirikie pale ulipojikwaa, siyo ulipoangukia.*
197. Ukali chambudza.  
*Ukali husababisha.*
198. Ukawe ufiche.  
*Kawia ufike.*
199. Ukulu wa meny'helo siyo ibugulu lya mifuwa.  
*Ukubwa wa pua siyo wingi wa makamasi.*



200. Uleche kubohola mhele hawele na ng'huku dzimuwile.  
 Uleche kubohola mhele halimipodzi minji.  
*Usimwage mchele penye kuku wengi.*

201. Uleche kujendela nyota ya miyago.  
*Usisafirie nyota ya mwenzako.*
202. Uliju ubao senga hele.  
*Linda kitu chako kisiondolewe.*
203. Usugu winji, kumwando gidza.  
*Ujanja mwingi, mbele giza.*




204. Usungu wa mwana yaudzelele yamulelile (mayimun'hu).  
*Uchungu wa mtoto aujuaye mzazi.*
205. Utaje ilala, ndzuchi dzikuleche.  
*Tupa sega, nyuki wakuache.*
206. Utaje lyo lile, mikondzi jikuleche.  
*Tupa lililooza, nzi wakuache.*

207. Vyeng'ha wing'ala siyo dzahabu.  
*Yote yang'aayo usidhani ni dhahabu.*
208. Wenye lukolo mwenda utitu.  
*Ndugu nguo nyeusi.*
209. Wibate! Wibate! Nagwe mbele.  
*Shika! Shika! Na mwenyewe nyuma.*




210. Widawe ng'hanu hananya.  
*Amka asubuhi na mapema.*  
*Ndege wa asubuhi hupata makuu (mazuri).*
211. Widzade moko, ho ufichila.  
*Jikune mkono unapofika.*
212. Winamidze, igoti lyokulonjela.  
*Inama, goti litakuambia.*
213. Winji siyo chin'hu.  
*Wingi si hoja.*

214. Wone huhuliche dzo wolonga wakulu, kabeneka mgulu.  
*Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.*




215. Wone huvidzelele kufa, ulole kabuli.  
*Ikiwa hujui kufa, tazama kaburi.*
216. Wone udwine kuluhengo, kodumila kulukandzi.  
*Kama utakimbia ukiwa chumbani, utaishia ukutani.*



217. Wone ugane kulya igubi, uhagule linenehe.  
*Ukitaka kula nguruwe, chagua aliyenona.*
218. Wone ugane kunyodzoka, milonjele na nyonga.  
*Ukitaka kuruka, agana na nyonga.*
219. Wone ugane mwino, ugane na ifulusa.  
*Kama ukipenda chumvi, upende na gunia lake.*
220. Wone uhuliche ny'hemo, kuna chin'hu.  
*Ukisikia mbiu, kuna kitu.*
221. Wone ukona hako halakala, ha muyago hangudakamila.  
*Ukiona kwako kunaungua, kwa mwenzako kunateketea.*

222. Wone ukuka haluga, wanyalaga lunyungu.  
*Ukiondoka nyumbani, panda mbegu za maboga.*
223. Wone ulapa kibata ng'huku, utodzele msele.  
*Ukitaka kukamata kuku, mtupie chenga.*



224. Wone ululeche lwate, kodzenga inji (ng'handा).  
*Usipoziba ufa, utajenga ukuta (nyumba).*
225. Wone ulya na chipofu, uleche kimibata moko.  
*Usile na kipofu, ukamshika mkono.*
226. Wone umpa mun'hu chin'hu, umugawile vyo ulinavyo,  
uleche kumugawila vyo ulihela.  
*Kama unampa mtu kitu, mgawie vile ulivyo navyo,  
usimgawie visivyo vyako.*
227. Wone udzenguhagulahagula, kohagula lyolile.  
*Kama unachaguachagua, unachagua lililooza.*

228. Wone wibate meli, limwe lyokulemwa.  
*Mshika mbili, moja humponyoka.*
229. Yadzowele kunyongotola, kudachila howedza.  
*Mzoea kunyonga, kuchinja hawezi.*



230. Yajendaga mp'hole mphole, hekwalaga.  
*Mwenda pole hajikwai.*
231. Yakumuliche nemisi, nechilo kokusoma.  
*Akumulikaye mchana, usiku atakuunguza (atakuchoma).*
232. Yali kufungo hogwilwa na igodi.  
*Aliye kando haangukiwi na mti.*
233. Yali na chilimbo chikali ndyo yatemaga nyama.  
*Mwenye kisu kikali ndiyeye alaye nyama.*
234. Yalihela mwana, yapape liganga.  
*Asiye na mwana aeleke jiwe.*
235. Yavumiliyaga kalyaga dzipile.  
*Mvumilivu hula mbivu.*

236. Yawele hela menji kana mado.  
*Asiye na mengi ana machache.*
237. Yawele na mong'ho mpise.  
Yawele na mwemvu kahela chilemedzwe.  
*Mwenye nguvu mpishe.*
238. Yegute hamdzelele yadagane.  
*Mwenye shibe hamjui mwenye njaa.*
239. Yetumbile cha mng'holodze kofa masichini.  
*Mtumaini cha ndugu hufa maskini.*



240. Yo chibatika na ngodzi yo muhidzi.  
*Mkamatwa na ngozi ndiyie mwizi.*
241. Yo haidzelele maana, halonjelagwa maana.  
*Asiyejua maana, haambawi maana.*

242. Yo hakudzelele, hokujali.  
*Asiyekujuja, hakuthamini.*
243. Yo hambi yawudze, kahela cho yochifundza.  
*Asiyeuliza, hanalo ajifunzalo.*
244. Yo umujesela yo yuyu, kumbe hebu.  
*Umdhaniaye ndiye, kumbe siye,*
245. Yodwina kochikwala chidole.  
*Mwenda mbio hujikwaa dole.*
246. Yogana vyeng'ha, kokosa vyeng'ha.  
*Mtaka vyote kwa pupa hukosa vyote.*
247. Yojenda hela siyo mkala hela, hanji kolokota.  
*Mtembea bure siyo mkaa bure, huenda ataokota.*
248. Yokuliga hokuhagulila iligo.  
*Akutukanaye, hakuchagulii tusi.*
249. Yokutadza kusida, yo miyago.  
*Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki. Anayekusaidia shida  
ndiye mwenzio.*
250. Yokuwinga, hokulonjela, uche.  
*Akufukuzaye, hakwambii, toka.*
251. Yolema wan'hu muhawi.  
*Anayekataa watu ni mchawi. Mkataa kikoa ni mchawi.*



252. Yolitogola idzuwa limwalichila.  
*Alisifuye jua limemwangaza.*
253. Yomwima mp'hanje, kampungudzila ufudzi.  
*Amnyimaye punda adesi kampunguzia (kamwepushia) mashuzi.*
254. Yopegwa ndiyo yonjedzagwa.  
*Apewaye ndiye aongezwaye.*
255. Yovina kuluga konolagwa.  
*Mcheza kwao hutuzwa.*
256. Yowinjigwa kuluga kwake kahela ha kuluta.  
*Mfukuzwa kwao hana pa kwenda.*
257. Yula hawele ngoneka, na mn'humbula kamu duhuli.  
*Asiyekuwapo na lake halipo. Asiyekuwapo machoni na moyoni hayupo.*

*Methali za Kiswahili kwa Kividunda*  
**N’helo dza Chiswahili kwa Chividunda**



1. *Akili imejificha.*  
Luhala mbundamile.
2. *Akili nyingi huondoa maarifa.*  
Luhala lwinji lyangusa maahalifa.
3. *Akili unayo utatembea, utaacha, inaenda.*  
Luhala kwa nalo kojenda, koleka, luluta.
4. *Akili ya mwenzio useme.*  
Luhala lwa miyago ulonje.
5. *Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.*  
Yokutadza kusida, yo miyago.
6. *Akufukuzaye, hakwambii, toka.*  
Yokuwinga, hokulonjela, uche.
7. *Akumulikaye mchana, usiku atakuunguza (atakuchoma).*  
Yakumuliche nemisi, nechilo kokusoma.
8. *Akutukanaye, hakuchagulii tusi.*  
Yokuliga hokuhagulila iligo.
9. *Alipolala kama zimwi, anakoenda, hujui*  
Ko yawasila kota idimu, ko undza mane.

10.




*Alisifuye jua  
limemwangaza.  
Yolitogola idzuwa  
limwalichila.*

11. *Aliye kando haangukiwi na mti.  
Yali kufungo hogwilwa na igodi.*




12. *Amka asubuhi na mapema.  
Widawe ng'hanu hananya.*

13. *Amnyimaye punda adesi kampunguzia (kamwepushia) mashuzi.*  
Yomwima mp'hanje, kampungudzila ufudzi.
14. *Anayekataa watu wengi ni mchawi*  
Yolema wan'hu muhawi.
15. *Anayekusaidia shida ndiyo mwenzio.*  
Yokutadza kusida, yo miyago.
16. *Apewaye ndiye aongezwaye.*  
Yopegwa ndiyo yonjedzagwa.
17. *Asiye na mengi ana machache.*  
Yawele hela menji kana mado.
18. *Asiye na mwana aelete jiwe.*  
Yалиhela mwana, yapape liganga.
19. *Asiyejua maana, haambiwi maana.*  
Yo haidzelele maana, halonjelagwa maana.
20. *Asiyekujua, hakuthamini.*  
Yo hakudzelele, hokujali.
21. *Asiyekuwapo na lake halipo. Asiyekuwapo machoni na moyoni hayupo.*  
Yula hawele ngoneka, na mn'humbula kamu duhuli.
22. *Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.*  
Wone huhuliche dzo wolonga wakulu, kobeneka mgulu.
23. *Asiyeuliza, hanalo ajifunzalo.*  
Yo hambi yawudze, kahela cho yochifundza.



24. *Avumaye baharini ni papa, kumbe wengine wapo.*  
Lidzeleche mmadzi menji li papa, kumbe jiyage jili kuko.

25.



*Bendera hufuata  
upepo.  
Bendela  
yangufata balidi.*

26. *Boga linakua haraka haraka, mwanzı hivyo hivyo.*  
Iyungu likulaga hima hima na idenje hihyo.
27. *Cha chini hukutana na cha juu.*  
Cha hasi chiting'anaga na cha mchany'ha.
28. *Cha mtu mavi (kinanuka nywele).*  
Cha mun'hu chinung'ha mvili.
29. *Cha mwenzio kitaalamu, umeze mate, ukalale.*  
Cha miyago chikangafu, umele mate, ukawase.

30.



*Chanda chema huvikwa*

*pete.*

*Chidole chinojile*  
*chovalidzwa pete,*

31. *Chombo kilichopikiwa samaki hakiachi kunuka vumba.*  
Chin'hu chiteleche somba, hachileka kunung'ha udzidziwa.



32. *Dalili ya mvua ni mawingu.*  
Chaluko cha n'honya ng'hungugu.

33. *Damu nzito kuliko maji.*  
Ndopa ndzito kuliko madzi.

34. *Dua mbaya haombolezewi mtoto (mwana).*  
Iduwa lihile hatambichidzagwa mwana.

35. *Dunia mti mkavu.*  
Isi igodi ikavu.


36. *Dunia tambara bovu, mwenye ngoma zake achaacheze.*  
Isi ibende, mwenye ngoma dzake uleche yadule.

37. *Fimbo ya mnyonge ni umoja.*  
Mboko ya mnyonje mulundo.
38. *Fumbo mfumbie mjinga mwerevu huling'amu.*  
Ifumbo mfumbile mpoka, yawele na luhala ama kalitanga.
39. *Haba na haba hujaza kibaba.*  
Tudo, tudo komemedza chidoto.  
Ndohe dza mp'hene dzivilaga kuching'onda.
40. *Hakuna msiba usio na mwenzake.*  
Kuduhu hajali ikosile miyage.



41. *Hakuna siri ya watu wawili.*  
Kuduhu sili ya wan'hu weli.
42. *Haraka, haraka haina baraka.*  
Hima, hima yahela mboto.

43. *Hasara humfika yule mwenye mabezo.*  
Hasala yomfika yula yawele nambedza.
44. *Hasira hasara.*  
Hasila hasala.
45. *Hasira za mkizi, furaha ya mvuvi.*  
Hasila dza mkidzi ny'hendze ya mlowaji.
46. *Hauchi, hauchi unakucha.*  
Hakucha, hakucha kucha.
47. *Heri kufa macho kuliko kufa moyo.*  
Heli ufe meho kuliko kufa n'humbula.
48. *Heri kujikwaa kidole kuliko kujikwaa ulimi.*  
Heli wikwale chidole kuliko kikwala lulimi.
49. *Hiari yashinda utumwa.*  
Hiyali yangusinda utumwa.
50. *Hucheka kovu asiyefikwa na jeraha.*  
Kanguseka ng'hovu yang'alifichikwa na chilonda.
51. *Hukunyima tongue, hakunyimi neno.*  
Kokwima n'honje, hokwima ineno.



52. *Ikiwa hujui kufa, tazama kaburi.*  
Kama huvidzelele kufa, ulole kabuli.


53. *Inama, goti litakuambia.*  
Winamidze, igoti lyokulonjela.
54. *Jambo usilolijua ni kama usiku wa giza.*  
Mbuli yo huidzelele ayo kota jidza ya nechilo.
- 55.



*Jembe halimtupi mtu  
(mkulima).  
Ihuka halimtagaga  
mun'hu.*

56. *Jifya moja haliinjiki chungu.*  
Ifigwa limwe halijeleva chiya.
57. *Jikune mkono unapofika.*  
Widzade moko, ho ukichila.
58. *Jina jema hung'aa gizani.*  
Itagwa linojile lyangung'ala kutitu.

59. *Jogoo wa kuazima anauma wakubwa na wadogo.*  
Idzogolo lyadzimwa lilumaga dzing'hulu na dzinyana.



60. *Jogoo wa shamba hawiki mjini.*  
Idzogolo lya kumugunda halikwika kump'hwani.
61. *Jungu kubwa halikosi ukoko.*  
Lukuwe lukulu halukosaga ukwangulo.
62. *Kaeni mnavyofahamiana.*  
Mikale vyo midzelele.
63. *Kama ukipenda chumvi, upende na gunia lake.*  
Wone ugane mwino, ugane na ifulusa.
64. *Kama unampa mtu kitu, mgawie vile ulivyo navyo,  
usimgawia visivyo vyako.*  
Wone umpa mun'hu chin'hu, umugawile vyo ulinavyo,  
uleche kumgawila vyo ulihela.
65. *Kama unachagua chagua, unachagua lililooza.*  
Wone udzenguhagulahagula, kohagula lyolile.
66. *Kama unakimbia ukiwa chumbani, utaishia ukutani.*  
Wone udwine kuluhengo, kodumila kulukandzi.

67. *Kamba hukatikia pembamba.*  
Ng'hweso hudumuchila hagandile.
68. *Kanga hazai ugenini.*  
Ikanga halilela kuujendzi.
69. *Kawia ufile.*  
Ukawe ufiche.
70. *Kazi mbaya si mchezo mwema.*  
Mijito jihile siyo mdawalo unojile.


71.




*Kidole kimoja  
hakivunji chawa.  
Chidole chimwe  
hachitulaga mp'hani.*

72. *Kigune ni cha karanga, njugu mawe hazina kigune.*  
Chigune cha mayowe, mp'helasi dzahela chigune.
73. *Kila mlango kwa ufunguo wake.*  
Chila lwidzi na funguwo yache.
74. *Kila mtoto na koja lake.*  
Chila mwana na likoja lyache.
75. *Kila ndege huruka kwa bawa lake.*  
Chila chideje changuguluka kwa ibawa lyache.
76. *Kilichotoka kwa mkarimu, upokee.*  
Chilawile kwa mutwa, ubochele.

77. *Kilio huanza mfiwa ndipo wa mbali waingie.*  
Chililo chalukaga yafililwe, leka wanji wa kutali wenjile.
78. *Kinu hakitwangwi bila kitu.*  
Ituli hawatwangaga bila chin'hu.



79. *Kinyesi cha mbuzi kinaongezeka kwenye zizi.*  
Midohe ja mp'hene jivilaga kuching'onda.  
Ndohe dza mp'hene dzivilaga kuching'onda.
80. *Kinyozi hajinyoi, akijinyoa, hujikata.*  
Mbeyaji hebeyaga, wone yebeye, kochitema.
81. *Kipendacho roho ni dawa.*  
Chigana n'humbula mkwandi.



82. *Kitanda usicholala hujui kunguni wake.*  
Chin'handa cho huwasile, hujidzelele mikugun'hi jake.

83. *Kitu kizuri kinaonekana, jua linapochomoza.*  
Chin'hu chinojile chonekaga, idzuwa lilawila.
84. *Kivuli cha fimbo hakimfichi mtu jua.*  
Chivuli cha ng'hweku chachimvisa mun'hu idzuwa.
85. *Kizuri chajuza, kibaya chajitembeza.*  
Chinojile changigudza, chichile changijendedza.
86. *Kosa moja haliachi mke.*  
Likosa limwe halilekaga mdala.
87. *Kuchamba kwingi, kutoka na mavi.*  
Kibiha kwinji, kokuka na mamvi.
88. *Kufa kwa mtu harusi.*  
Kufa kwa mun'hu halusi.
89. *Kuishi kwingi ni kuona mengi.*  
Kikala kwinji, kolola menji.
90. *Kujikwaa si kuanguka, bali ni kwenda mbele.*  
Kikwala siyo kugwa, kuluta kumwando.
91. *Kukombeleza siyo sawa na kukosa kabisa.*  
Ng'hombeledza si sawa na chibalu.
92. *Kuku havunji yai lake.*  
Ng'huku haitulaga ifinga lyache.
93. *Kuku mgeni hakosi kamba mguuni.*  
Ng'huku njendzi haikosaga ludzabi muludzayo.
94. *Kuku mwenye watoto halengwi jiwe.*  
Ng'huku iwele na wana haitodzelagwa iganga.

95.




*Kulea mimba siyo  
kazi, kazi kulea  
mtoto.*

Kutundza himila  
siyo mjiito, mijiito  
kutundza mwana.

96. *Kupotea njia ndiyo kujua njia.  
Kwajilila ndzila ndo kuidzela ndzila.*

97. *Kutoa ni moyo, si utajiri.  
Kulavya chin'hu n'humbula, siyo utajili.*



98. *Kutupa jongoo na mti wake.  
Kuhomba igwingwi na igodi lyake.*

99. *Kuuliza si ujinga.  
Kuwudza siyo upoka.  
Mawudza halyaga cha mun'hu.*

100. *Kuvuja kwa pakacha nafuu ya mchukuzi.*  
Kuhulula kwa idebe mp'humu ya mpikaji.
101. *Kwenda mbio siyo kufika.*  
Kuluta hima hima siyo kufika
102. *La juu halitunguliwi.*  
Lya mchany'ha halitungulagwa.
103. *Leo ni leo, asemaye kesho ni mwongo.*  
Lehano yo lehano, yolenga cheso mdesi.
104. *Lililopita mara moja, halitegwi.*  
Likwete, kamwe halitegagwa.
105. *Linda kitu chako kisiondolewe.*  
Uliju ubao senga hele.
106. *Lisemwalo lipo, ikiwa halipo, lipo nyuma, linakuja.*  
Lilonjigwa lya kuko, wone likuduhu, lya kumbele,  
lyanguya.
107. *Macho hayana pazia.*  
Meho gahela paziya.
108. *Maji ya kifuu, bahari ya chunguchungu.*  
Madzi ga chiwambu, bahali ya misungusungu.
109. *Mapenzi ni kikohozi, hayawezi kufichika.*  
Mapendzi ng'hololo, hogowedza kivisa.
110. *Maskini haokoti, akiokota huambiwa kaiba.*  
Masichini halokotaga, wone yalokote, wota kahidza.
111. *Mavi ya kale hayanuki.*  
Mamvi ga katali haganung'haga.
112. *Mbaazi ukikosa maua, husingizia juu.*  
Mp'hanje wone iwe hela mavuwa, yangusinjidzia idzuwa.



113. *Mbuzi mkiwa anajichunga peke yake.*  
Kapene kachiwa kedimaga kali yeng'ha.
114. *Mbuzi sehemu ya kulamba hakosi kwenda.*  
Mp'hene kuching'wenyo haikosaga kuluta.



115. *Mchagua jembe hajui kupiga jembe (si mkulima).*  
Mhagula ihuka hadahile kutowa ihuka.

116. *Mchagua nazi hupata koroma.*  
Mhagula nadzi kokwinula mbowa.
117. *Mchawi mpe mwana, alee.*  
Mhawi umupe mwanago, yahembule.
118. *Mchele mmoja, mapishi mengi.*  
Muhele umwe, utelekaji wenji.
119. *Mchele mmoja, mapishi mbalimbali.*  
Muhele umwe, utelekaji wahlenji.
120. *Mcheza na tope humrukia.*  
Mdawalila midongo jomnyondzo chela.
121. *Mcheza kwa hutuzwa.*  
Yovina kuluga konolagwa.




122. *Mchimba kisima huingia mwenyewe.*  
Mbawa chisima kokwinjila yuye.
123. *Mchovya asali hachovyi mara moja.*  
Mdovya hanombwa hadovyaga kamwe.
124. *Mchoyo hana marafiki (hana ukoo).*  
Mbuhu kahela lukolo.
125. *Meno ya mbwa hayaumani.*  
Mibogogo ja libwa halijilumaga.


126. *Mfanya ovyo akaondoka, anayefanya vizuri akala.*  
Mkola maya koka, kasejeda, kalya.
127. *Mfanyia juani atalia kivulini.*  
Mkolela midzuwa kodila mchimbehelo.
128. *Mfukuzwa kwao hana pa kwenda.*  
Yowinjigwa kuluga kwake kahela ha kuluta.
129. *Mfyeka migomba masilahi yake yamo ndani.*  
Muhenjela ng'howo igofu lya mugati.
130. *Mganga hajigangi.*  
Mganga hedzundzuwikaga.
131. *Mgongo unaokubeba ndiyo utakaoulilia.*  
Mgongo ukupapaga ndiyo koullilila.
132. *Mgonjwa haulizwi uji.*  
Mtamiche haudzagwa ibwembwela.
134. *Mjumbe hauawi.*  
Chitumagwa hakopolagwa.



135. *Mjusi na pango lake.*  
Mdusu na mp'halika yake.




136. *Mkamatwa na ngozi ndiye mwizi.*  
Yo chibatika na ngodzi yo muhidzi.
137. *Mkataa kikoa ni mchawi.*  
Yolema wan'hu muhawi.




138. *Mkono mtupu haulambwi.*  
Moko yeng'ha haumyangagwa. Moko uliyeka  
hawamyangaga.

139. *Mkulima mmoja, walaji wengi.*  
Mlimaji yumwe, walyaji ibugulu.
140. *Mla asali atamaliza kibuyu.*  
Mulya hanombwa komalidza ibuyu.
141. *Mmeza mengi, koo pana.*  
Mmela minji, lumelo lugadzi.
142. *Mkuki kwa nguruwe, kwa binadamu mchungu.*  
Imaka uhome kwa mun'hu lya usungu.



143. *Mnyama mkimya ndiye anayepata chakula.*  
Ing'oko linyamalile lo lipataga ndiya.
144. *Mpanda ovyo hula ovyo.*  
Mnyala vibi kolya vibi.

145. *Mpishi wa dawa hajitibu mwenyewe.*  
Mteleka mikwandi hetele kaga yuye.
146. *Mshika mbili, moja humponyoka.*  
Mbata meli, limwe lyomulemwa. Wone wibate meli,  
limwe lyokulemwa.
147. *Mtaka vyote hukosa vyote.*  
Yogana vyeng'ha kokosa vyeng'ha.
148. *Mtembea bure siyo mkaa bure, huenda ataokota.*  
Yojenda hela siyo mkala hela, hanji kolokota.



149. *Mto mdogo umejaa mamba.*  
Kadzanda kado kamema mimamba.
150. *Mtoto hatunzwi kwenye nyumba ya mwenzako.*  
Mwana hatundzilagwa mng'anda mwa miyago.
151. *Mtoto kunya kande, katafuniwa na mama yake.*  
Mwana kanya ng'hande, kadakulilwa na mayake.

152. *Mtoto umleavyo, ndivyo akuavyo.*  
Mwana wone umudime, kokula hihyo.
153. *Mtoto wa nyoka ni nyoka.*  
Mwana wa idzoka idzoka.
154. *Mtu hakatai wito, hukataa neno.*  
Mun'hu halemaga kuchemigwa, kolema cho yochemelwa.
155. *Mtu mwenye shida mlinzi wake Mola.*  
Chikunde mbala mwamidzi Mulungu.
157. *Mtumaini cha ndugu hufa maskini.*  
Yetumbile cha mng'holodze kofa masichini.
158. *Mume wa mama ni baba.*  
Mulume wa mamo yo baba.
159. *Mungu hamfichi mnafiki.*  
Mwenyegawa hamvisaga mnafichi.



160. *Mvua kubwa zote zina mbu.*  
N'honya ng'hulu dzeng'ha dzina ndzugun'hi.

161. *Mvumilivu hula mbivu.*  
Yavumiliyaga kalyaga dzipile. Ing'oko linyamalile lo lipataga ndiya.
162. *Mvunja nchi ni mwananchi.*  
Mbenza isi ni mwanaisi.
163. *Mwenda mbio hujikwaa dole.*  
Yodwina kochikwala chidole.



164. *Mwenda pole hajikwai.*  
Yajendaga mp'hole mphole, hekwalaga.
165. *Mwenye kisu kikali ndiye alaye nyama.*  
Yali na chilimbo chikali ndyo yatemaga nyama.
166. *Mwenye nguvu mpishe.*  
Yawele na mong'ho mpise.  
Yawele na mwemvu kahela chilemedzwe.
167. *Mwenye shibe hamjui mwenye njaa.*  
Yegute hamdzelele yadagane.
168. *Mwenyezi Mungu anajua peke yake.*  
Mulungu kedzela yeka.

169. *Mwenzako akinyolewa, zako tia maji.*  
Muyago wono yobeigwa, nagwe udodze madzi.
170. *Mwiba ulipoingilia ndiyo hapo utakapotokea.*  
Lupogo ho lwinjilile ndiyo baho ho lulawila.
170. *Mwizi hushikwa na mwizi mwenzake.*  
Mhidzi kochibatika na mhidzi miyage.
171. *Mzaha mzaha hutumbuka usaha.*  
Mbedzambedza jotumbuka mifila.
172. *Mzigo wa mwenzio ni kanda la sufi.*  
Ifulusi lya miyago ni chikanda cha sufi.
173. *Mzoea kunyonga, kuchinja hawezi.*  
Yadzowele kunyongotola, kudachila howedza.
174. *Nchi iliyokosa wakubwa inakosa ustawi.*  
Isi ilihela wakulu, haiwaga.




175. *Ndege hutua kwenye miti aupendao.*  
Chideje chigwaga migodi ho chiganile.



176. *Ndege mjanja hunaswa kwenye tundu bovu.*  
Chideje chisugu chogwilila mchitubuli chihalibiche.
177. *Ndege wa asubuhi hupata makuu (mazuri).*  
Widawe ng'hanu hananya.
178. *Ndizi kipakapaka zimeiva, watu wanashindwa kula.*  
Ng'howo chipakapaka dzipy'a, wan'hu wangulemwela kulya.
179. *Ndugu nguo nyeusi.*  
Wenye lukolo mwenda utitu.
180. *Ngojango yaumiza matumbo.*  
Kubetedzabetedza kwangulumidza munda.
181. *Nguruwe kafa, kachongewa.*  
Ngubi kafa, kana mgonedzi.
182. *Nisaidie kwenye juu. Kesho nitakusaidia kwenye mvua.*  
N'hadze kuli idzuwa. Cheso ndokutadza kuli n'honya.

183. *Nyani na tumbili na msitu wao.*  
Nyani na n'humibili na muhulo wao.
184. *Nyuki wakali wana asali.*  
Ndzuchi ng'hali ina ulengu.
185. *Nzi hufia kwenye kidonda. Ng'hondzi ifilaga mchilonda. Ng'hondzi kufila mchilo siyo vibi.*
186. *Pabaya pako si pema pa mwenzako.*  
Hehile hako siyo hanojile ha miyago.



187. *Paka akiondoka, panya hutawala.*  
Inyau wone lyuche, igule lyohalila.
188. *Pania nguo, uende huku na kule, watu watakusifu.*  
Ikune ibende, ujende nimwanimwa, wan'hu wakutogole.
189. *Panya wengi hawachimbi shimo.*  
Mibewa minji hajibawaga mwina ulute.
190. *Penye machungu baadaye pana chakula.*  
Hali usungu hamwaka hana chilyo.
191. *Penye mafundi hapakosi wanafunzi.*  
Hawele na wadahile hawakosaga wakifundza.

192. *Penye miti mingi hakuna wajenzi.*  
Kuli migodi minji wan'hu wa kudzenga kuduhi.
193. *Penye nia pana njia.*  
Halina luhuwi, hana ndzila. Hawele na niya, ndzila yowa baho.



194. *Penye wazee haliharibiki neno.*  
Hawele na wadzehe haiharibikaga mbuli.
195. *Pilipili usiyoila yakuwashiani?*  
Chidzanga cho hudile chokwawa choni?




196. *Polepole ndiyo mwendo.*

Mp'hole mp'hole mwandza wangutulika.

197. *Pombe ya kuuza haiishi.*

Ujimbi ngule haumalaga.



198. *Samaki mkunje angali mbichi.*

Somba uibine ing'hali ndodi.

199. *Shamba dogo limelimwa na watu wengi.*  
Kagunda kado kalimwa na wan'hu wenji.
200. *Sheria ni msumeno, hukata huku na huku.*  
Seliya musumeno, wangutema kuno na kuno.
201. *Shika! Shika! Na mwenyewe nyuma.*  
Wibate! Wibate! Nagwe mbele.
202. *Shimo la nyoka lina woga, shimo la panya buku tuko wote.*  
Mwina wa ndzoka wawoga, mwina wa mbuku twa hamwe.
203. *Shoka lisilo na mpini halichanji kuni.*  
Iwago lilihela chaka haitema ngodi.



204. *Shukrani ya punda mateke.*  
Malumbo ga idogowi mateche.
205. *Sikio halilali na njaa.*  
Isichiyo haliwasaga na ndzala mwemvu.
206. *Siku njema huonekana asubuhi.*  
Siku igoloche yonekaga usubuhi.

207. *Siku utakayokwenda uchi, ndiyo siku utakayokutana na mkweo.*  
Siku yo ujenda mwadzi, mo chiting'ana na mkweyo.
208. *Siku za mwizi ni arobaini.*  
Mhidzi siku dzache alubayini.




209. *Simba wawili hawapokonywi nyama.*  
Simba mbili habokwa nyama.
210. *Siyo kila mwenye makucha huwa ni simba.*  
Siyo jeng'ha jiwele na midole jiwaga misimba.
211. *Teke la kuku halimuumizi mwanawe.*  
Ng'huku wone ibije mwanage, hafaga.
212. *Tembea, uone nchi, ina matatizo.*  
Ujende, ulole isi, ina kwalo.
213. *Tupa lililooza nzi wakuache.*  
Utaje lyo lile, mikondzi jikuleche.

214. *Tupa sega, nyuki wakuache.*  
Utaje ilala, ndzuchi dzikuleche.
215. *Twende, twende tunavyoenda.*  
Dzuko, dzuko vyotulutaga.




216. *Uchungu wa mwana aujuaye mzazi.*  
Usungu wa mwana yaudzelele mayimun'hu.  
Usungu wa mwana yaudzelele yamulelile.
217. *Ujanja mwingi mbele giza.*  
Usugu winji kumwando gidza.

218. *Ukali husababisha.*  
Ukali chambudza.
219. *Ukarimu unaliwa.*  
Udeche ulyagwa.
220. *Ukasirikie pale ulipojikwaa, siyo ulipoangukia.*  
Ukalalile hoikwalile, siyo hougwile.
221. *Ukiona kwako kunaungua, kwa mwenzako kunateketea.*  
Wone ukona hako halakala, ha muyago hangudakamila.
222. *Ukiondoka nyumbani, panda mbegu za maboga.*  
Wone ukuka haluga, wanyalaga lunyungu.
223. *Ukishirikiana na walioshiba (watakomba), watacumalizia mboga.*  
Kohanga na wegute (wokukombela), wokusindila mboga.
224. *Ukisikia mbiu, kuna kitu.*  
Wone uhuliche ny'hemo, kuna chin'hu.
225. *Ukitaka kukamata kuku, mtupie chenga.*  
Wone ulapa kibata ng'huku, utodzele msele.




226. *Ukitaka kula nguruwe, chagua aliyenona.*  
Wone ugana kulya igubi, uhagule linenehe.

227. *Ukitaka kuruka, agana na nyonga.*  
Wone ugana kunyodzoka, milonjele na nyonga.
228. *Ukubwa wa pua siyo wingi wa makamasi.*  
Ukulu wa meny’helō siyo ibugulu lya mifuwa.
229. *Ulikoshinda ndiko utapata chakula.*  
Ko uswese, ko ulya.
230. *Ulimi unatafuna kuliko meno.*  
Lulimi lyangujejeda kuliko mibogogo.
231. *Umdhaniaye ndiye, kumbe siye.*  
Yo umujesela yo yuyu, kumbe hebu.
232. *Ungalijua alacho nyuki usingalionja asali.*  
Nauchidzele cho ilya ndzuchi, hawalijedza hanombwa.
233. *Upele hupewa, usikucha.*  
Mibadzuka jimugwaga mun’hu yалиhela ndole dza kidzadila.
234. *Upendalo hupati, hupata ulijaliwalo.*  
Lyō uligana hulipata, kolipata lila lyō wandichilwe.
235. *Usile na kipofu, ukamshika mkono.*  
Wone ulya na chipofu, uleche kimibata moko.



236. *Usimwage mchele penye kuku wengi.*


Uleche kubohola mhele hawele na ng'uku dzimuwile.  
Uleche kubohola mhele halimipodzi minji.



237. *Usipoziba ufa, utajenga ukuta.*

Wone ululeche lwate, kodzenga inji.

238. *Uasisafirie nyota ya mwenzako.*  
Uleche kujendela nyota ya miyago.



239. *Usitupe jongoo na mti (mpera) wake.*  
Kotaga ng'hwabi na ipela lyake.  
Kuhomba igwingwi na igodi lyake.



240. *Uso umeumbwa na haya.*  
Kumeho kuwumbigwa na soni.
241. *Utachokonoa lililoko kwenye pango, litatoka, litakuumma.*  
Kosoka lili mp'halika, lyolawa, lyokulumwa.
242. *Utajikuna pasipokunwa.*  
Kochidzada ha hadzadagwa.

243. *Utakuwa utaviona, ukubwa hauchezi.*  
Kokula kovyona, ukulu hauvinaga.

244. *Utapiga, bado halijatoka.*  
Kotowa, halinalawa.



245. *Vita vy a panzi furaha ya kunguru.*  
Kisubula kwa mipandzi ny'hendze dla mibondwa.



246. *Waarabu wa Pemba hujuana kwa vilemba.*  
Mun'hu na miyage wedzela kwa miwende jawo.

247. *Wingi si hoja.*  
Winji siyo chin'hu. Ibugulu siyo chin'hu.
248. *Ya kale hayapo.*  
Ga katali, ga kuduhi.
249. *Yote yang 'aayo usidhani ni dhahabu.*  
Vyeng'ha wing'ala siyo dzahabu.
250. *Zimwi likujualo halikuli, likakwisha.*  
Lidimu likudzelele halikulya, lisinde.